

Usawiri wa Nguvu-uhai katika Jamii za Kiafrika: Mifano Kutoka katika Riwaya ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*

Atupele Kamage

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

Ikisiri

Nguvu-uhai ni kipengele muhimu katika falsafa ya maisha ya Waafrika na kitu muhimu kinachofanya tajiriba za Waafrika. Msukumo wa kuchunguza Nguvu-uhai katika jamii za Kiafrika kupitia riwaya ya Kiswahili unatokana na kuwapo kwa madai kuwa msingi wa jamii za Kiafrika kuamini kuwa viumbe vyote vina roho au uhai haukidhi kanuni za kimantiki na umepitwa na wakati (Smith, 1961). Hii ina maana kuwa Nguvu-uhai huchukuliwa kwa mitazamo tofauti kutegemeana na tajiriba na imani za kijamii. Kutokana na tofauti hizo za kimtazamo, tuliona ipo haja ya kuchunguza Nguvu-uhai katika jamii za Kiafrika ili kubainisha ujitokezaji wake katika riwaya za Kiswahili. Ili kutimiza azma hiyo ya utafiti huu riwaya ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi* ilirejelewa. Data kutoka maktabani zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na uhakiki wa riwaya teule. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Kwa kutumia mkabala wa kitaamuli data zilichambuliwa, zilichakatwa na kuwasilishwa. Matokeo yanaonesha kwamba Nguvu-uhai ni dhana pana katika jamii za Kiafrika na hugusa nyanja zote za maisha yao. Baadhi ya nyanja hizo ni kama vile na mila na desturi, maadili, afya ya jamii na uzazi. Kupitia vipengele hivyo maudhui mbalimbali kuhusu Waafrika huelezwa.

Maneno Muhimu: *Nguvu-uhai, Ontolojia ya Kiafrika*

Utangulizi

Makala haya yamechunguza usawiri wa Nguvu-uhai¹ katika jamii za Kiafrika kwa kurejelea riwaya ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi* (1967). Kwa mujibu wa wanazuoni wa Kimagharibi, Nguvu-uhai kwa Waafrika ni imani ambazo zimejengwa katika nguvu mbalimbali na kwamba viumbe vyote vina roho (Tempels, 1959; Smith, 1961; Tylor, 2010). Wataalamu wenye mtazamo huu walipoitazama dhana ya Nguvu-uhai walidai kuwa haikidhi kanuni za kimantiki. Baadhi yao wametoa kauli na hata kufikia hatua ya kuihusisha dhana hii na masuala yanayohusu uchawi na ushirikina. Tempels, Smith na Tylor (wameshatajwa) wanaeleza kuwa kuamini katika vitu hivi ni uovu.

Kutokana na mtazamo huo wa Kimagharibi, baadhi ya wataalamu wenye mtazamo wa Kiafrika walikemea na kupinga mtazamo huo wa kuhusisha Nguvu-uhai na matendo ya kiuchawi na kiushirikina wakadhihirisha hisia zao kupitia kazi walizoandika. Kupitia maandiko hayo, maana ya Nguvu-uhai ilielezwa na kubainika. Walijaribu kuelezea matendo, hasa mila na tamaduni za Waafrika na jinsi Nguvu-uhai inavyobainika (Mbiti, 1969; P'Bitek, 1970). Mbiti na P'Bitek wanasisitiza kuwa Nguvu-uhai kwa Waafrika zimefungamana na imani za kidini na matendo mbalimbali. Hivyo, ni vema imani hizi zikaeleweka na kutafsiriwa kwa kuzingatia muktadha wa Kiafrika. Mtazamo huu baadaye ulipaliliwa na kuchochewa na wataalamu wengine kama Magesa, 1997; Nkemnkia, 1999; Mihanjo, 2007; Nalwamba na Buitendag, 2017; Ngangah, 2019; na Agada, 2020) walioelezea kuwa Nguvu-uhai ni kitu chenye thamani katika maisha ya Waafrika na ndio utambulisho wao. Pia, walieleza kuwa matendo yote yanayofanyika katika mzunguko wa maisha ya Waafrika huhusisha suala la Nguvu-uhai, na hupata maana katika muungano unaojumuisha vitu mbalimbali kama vile miungu, mizimu, viumbe, asili na vitu mbalimbali.

¹ Nguvu-uhai ni nguvu ya pekee inayofanya tajiriba za Waafrika. Nguvu hii haionekani kwa macho bali huhusiwa tu na kuaminika kuwa hupatikana kwa kila kiumbe.

Katika jamii za Kiafrika Nguvu-uhai hudhihirika katika matendo mbalimbali katika maisha ya mtu tangu kuzaliwa mpaka kufa kwake. Nguvu hizo hudhihirika kupitia ulimwengu unaoonekana na usioonekana na huweza kumstawisha ama kumdhoofisha binadamu. Nguvu hizo husambaa katika viumbe kupitia uhusiano wa ndani ya kiontolojia. Nguvu hizo ni za ndani na zinaonesha namna binadamu kama kiumbe ambaye hawezi kuishi peke yake bila kujihusisha na viumbe wengine kwa sababu viumbe vyote vinahusiana kupitia muumba wao mmoja ambaye ndio chanzo muhimu cha nguvu zote na uhai, kila kimoja kinahusiana na kingine na kwa ontolojia kimeunganika. (Mihanjo, 2004). Mwanafalsafa Mbiti, (1969) anabainisha kuwa Mwafrika anayo maoni ya ukweli ambayo ni pamoja na Mungu, roho, mtu, wanyama na vitu mbalimbali vinavyotambulika na hisia na ambavyo havina uhai wa kibaolojia. Mfumo wa ngazi wa vitu hivyo ni umoja na mshikamano wao ambao unatengenezwa na Umungu na unapenywa na nguvu isiyoelezeka, uwezo au juhudi ambayo siyo lazima iwe Nguvu-uhai katika tafsiri ya kibailojia ila inayopaswa kueleweka kwa ajili ya metafizikia ambayo inawaunganisha viumbe na muumbaji wao. Hivyo, Mwafrika anapoyataja majina ya vitu mbalimbali, wanyama au watu, mara kwa mara anakuwa na maana pia ya nguvu asili ya Mungu iliyomo katika viumbe hivyo. Jina la kitu chochote kisicho na uhai au kitu cha asili kama vile jua, linaweza kutumika kuelezea nguvu zisizoelezeka za Mungu ambazo hupitishwa katika kitu hicho.

Kwa maana hiyo, Waafrika wanaunganisha nguvu za ndani za kiontolojia zinazoimarisha uhusiano wao na nguvu nyingine. Ijapokuwa uwepo wake hauwezi kuonekana (kwa sababu hazina umbo), haupo mbali na binadamu. Nguvu hizi zinaweza kuendesha maisha na hata kutoa adhabu iwapo mtu atakiuka taratibu za kimaadili (Lavenda na Schultz, 2010). Lavenda na Schultz wanadai kuwa binadamu akizitumia vizuri huweza kupata faida. Ndiyo maana, Nkemnkia (1999) anaeleza kuwa Nguvu-uhai inahusu mambo yote katika maisha ya Mwafrika pasipo kuweka mipaka kati ya imani za kidini na maisha ya kila siku, roho na mwili pamoja na dunia ya walio hai na wafu. Kwa hiyo, kwa Waafrika kila kitu ni Nguvu-uhai. Kwa ufupi, Nguvu-uhai kwa Waafrika ni muunganiko wa kila kitu kinachoonekana na kisichoonekana kwa macho ulimwenguni. Ulimwengu kama uwanja wa nguvu mbalimbali unaainisha mfumo wa tabaka za nguvu hizo. Mungu ndiyo nguvu kuu juu ya nguvu zote, akifuatiwa na wahenga, mahoka na mizimu; mtu, na chini kabisa vitu vyote visivyo na uhai (Mihanjo, 2004). Kimsingi, wanadamu daima wanashawishiana, wanavutiana, au moja kwa moja kwa kukusudia au pengine bila kukusudia bali kwa nguvu zisizo za kibinadamu au kwa kutumia wahenga. Kwa hiyo, madai ya kuhusisha Nguvu-uhai na kuifungamanisha na vitendo vya uchawi na ushirikina yanaleta ukakasi kwa jamii. Aidha, tafiti chache zilizofanywa kuhusu Nguvu-uhai hazijakitwa katika misingi ya kinadharia hivyo kufinya, mawanda yake. Isitoshe, Mpalanzi (2019) anaeleza kuwa utafiti kuhusu Nguvu-uhai katika fasihi ya Kiswahili unahitajika kufanyika kwa kina ili kuweza kuelewa mawanda yake. Kwa kuwa Nguvu-uhai huelezea mambo yote kwa Waafrika, huonekana katika fasihi na hata sanaa zao. Hivyo, kwa kuwa kuwa fasihi haitoki katika ombwe huakisi yale yanayotendeka katika jamii tuliona haja ya kufanyika uchunguzi ili kuziba pengo hili. Kutokana na hali hii makala haya yamebainisha vipengele vya Nguvu-uhai katika riwaya teule ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*.

Makala haya yanalenga kuchunguza Nguvu-uhai kama inavyosawiriwa katika jamii za Kiafrika kwa kutumia Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Makala haya yanadai kuwa ili kuilewa vizuri dhana ya Nguvu-uhai, msomaji anapaswa kuilewa vema Ontolojia ya Kiafrika kwa sababu dhana hii hueleweka kwa kuhusisha na dhana nyingine. Ndio maana, kwa Waafrika Nguvu-uhai ni kitu ambacho hakikamatiki kwa mikono, wala kuonekana bali huhisiwa tu. Katika mjadala huu, tutajadili usawiri huo huku tukibainisha uhusiano wa usawiri huo na Ontolojia ya Kiafrika.

Utafiti huu ni wa maktabani. Maktaba zilizotumika ni maktaba ya Dkt. Wilbert Chagulaya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maktaba ya Taasisi za Taaluma za Kiswahili na Makavazi yake (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika maktaba hizi mtafiti alizitumia katika kusoma nyaraka mbalimbali na kukusanyia data zinazohusiana na makala haya.

Data za makala haya zimechambuliwa kwa kuzingatia Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Mawazo ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika² yaliasisiwa kwa mara ya kwanza na Tempels katika karne ya 20 alipoandika kitabu chake cha *Bantu Philosophy* (1959). Ontolojia ya Kiafrika ni nadharia inayozungumzia mawazo ya Waafrika kuhusu kuwapo kwa vitu katika dunia na kuangalia uasili wa vitu hivyo. Ontolojia haichunguzi tu maana ya kuwapo bali huchunguza pia suala la Nguvu-uhai ambalo ndilo linafanya kuwapo kwa Waafrika. Tempels (1959) aligundua kuwa kuwapo kwa Waafrika kumejengwa na kitu kinachoitwa Nguvu-uhai. Nguvu-uhai hii, ndiyo inayotawala maisha yote ya Waafrika. Anaeleza kuwa nguvu haitengani kamwe na kiumbe hai na kwa sababu hiyo mawazo haya mawili yanabaki yanashikamana pamoja katika kumwelezea kiumbe hai. Waafrika wanaamini kwamba viumbe wanadumisha uhusiano baina yao, uhusiano wa ndani wa ontolojia unaolingana na mshikamano nasibu wa muumba wao. Kwa hiyo, kiumbe au binadamu siyo tu yupo bali hasa “yupo kwa kuwa na nguvu” au anafanya kitu. Ingawa nguvu hiyo ni asili au halisi kwa kiumbe, lakini chanzo chake au msingi wake unatoka nje (Mihanjo, 2004). Hivyo, nguvu yoyote anayopewa kiumbe au binadamu anaipata kutoka kwa kiumbe mwenye cheo kikubwa zaidi, kiumbe bora zaidi, ambaye kwa ndani na nje anayo nguvu hiyo.

Baada ya utafiti wa Tempels (1959) wanazuoni mbalimbali wamejitokeza na kuchangia mjadala kuhusu Ontolojia ya Kiafrika. Wanaeleza kuwa katika Ontolojia ya Kiafrika Nguvu-uhai huhusu masuala mengine ambayo huaminika kuwa yana athari katika maisha ya Waafrika (Parrinder, 1969; Mbiti, 1969; Tugendhat, 2016; Mulokozi, 2017; Ngangah, 2019). Kwa mantiki hiyo, Ontolojia ya Kiafrika inajumuisha mambo mbalimbali ya Kiafrika ambayo kupitia kwazo mawazo hutolewa yakielezea maana ya maisha kwa Waafrika na jinsi Waafrika wanavyoyatumia mawazo hayo kuutafsiri ulimwengu wao. Wataalamu hawa wanaainisha vipengele mbalimbali ambavyo vinaweza kutumika kama muongozo katika kuhakiki kazi za fasihi ili kuilewa vema Ontolojia ya Kiafrika. Kipengele cha kwanza, ni dhana ya maadili. Masolo (2011) anaeleza kuwa ubora wa maadili na matendo ya kibinadamu ndiyo muundo wa Ontolojia ya Waafrika, na hutegemea iwapo matendo hayo yanachangia katika kuleta au kuharibu usalama katika mfumo wa Nguvu-uhai. Matendo yanayoleta usalama huchukuliwa kuwa maadili. Matendo yanayoharibu huchukuliwa kuwa maovu. Kwa Waafrika maadili huhusu vipengele mbalimbali kama ukweli, upendo, heshima kwa wengine na mali zao, kutunza makubaliano, kutimiza wajibu, staha na utii katika jamii. Kipengele cha pili, kuthamini uzazi na imani kuwa mwanadamu akikosa uzazi ni laana. Uzazi ukikosekana basi mfumo huu wa maisha hautakuwepo. Uzazi unaendelea Nguvu-uhai ili maisha yaendele, hivyo, ni lazima uzazi upatikane. Kutokuzaa kwa Waafrika kuna maana ya kuzuia mkondo wa maisha. Kipengele cha tatu, ontolojia hii inashikilia kwamba kuna uhusiano baina ya kiumbe na kiumbe, yaani baina ya nguvu na nguvu. Binadamu yeyote yule, haishi peke yake ila ni mmoja katika ontolojia ya uhai ambayo anahusiana nayo, na huiathiri na kuathiriwa nayo. Katika mahusiano haya, Waafrika wanatambua kuwa mtu hawezi kuishi peke yake bali anapaswa kuhusiana na watu, kabila lake au ukoo wake, uhusiano na viumbe wengine, mahusiano na wanyama na vitu vinavyomzunguka. Mfungamano huu hudumisha uhusiano wa ndani wa kiontolojia unaolingana na mshikamano nasibu baina ya viumbe na Mungu. Mungu ndiye kiini cha nguvu zote za ulimwengu.

Maadili, kuthamini uzazi, mahusiano na ushirikiano baina ya viumbe wengine walio hai na wafu, ni baadhi ya masuala yanayotoa mwanga kuhusu usawiri wa Nguvu-uhai. Makala haya yameonesha usawiri wa Nguvu-uhai katika jamii za Kiafrika kwa kutoa mifano kutoka riwaya teule ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*.

Nguvu-uhai katika Jamii za Kiafrika

Matokeo ya data zilizochunguzwa yamewasilishwa kwa kadiri inavyowezekana katika sehemu hii. Uwasilishaji sawia unafanyika kwa kuzingatia lengo mahususi la makala. Vipengele vilivyobainishwa

²Ontolojia ya Kiafrika inazungumzia maarifa, mtazamo na imani ya jamii kuhusu maisha na kuwapo kwake na kuhusu ulimwengu kwa ujumla. Pia Ontolojia ya Kiafrika inatambuliwa na wanazuoni wengine kama Ontolojia ya Kibantu. Licha ya tofauti za kimawanda, lakini maana, misingi na matumizi huwa linganifu (Mulokozi, 2017).

na makala haya ni mila na desturi, maadili, afya na uzazi. Sehemu inayofuata imewasilisha namna kipengele cha Nguvu-uhai kinavyosawiriwa katika riwaya teule.

Mila na Desturi

Madumulla (1998) anaeleza kuwa mila ni hali ya kudumu ya maisha ya kila siku ya watu ambayo inahusu sana asili ya watu. Mila hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi na kuthaminiwa sana na watu kama dira ya maisha yote ya jamii. Mila hujumuisha mambo mengi kama malezi ambayo huonekana katika miiko, historia, matibabu, heshima, maadili, taratibu za jamii zihusuzo masuala ya ndoa, uzazi, vifo, mazishi na urithi. Mila katika jamii za Kiafrika huchukuliwa kama ndio katiba ya kuongoza jamii (Madumulla, 1998). Desturi ni mazoea ya matendo ambayo yanaweza kubadilishwa na baadaye kupokelewa kama mila ya jamii Mila na desturi hizi hutofautiana kati ya jamii moja na nyingine kutegemeana na mazingira. Mila na desturi hujumuisha lugha, itikadi, sanaa, mshikamano, sheria au taratibu fulani zinazofuatwa na jamii. Utafiti huu umebaini kwamba, Nguvu-uhai hujitokeza sana katika masuala ya mila na desturi za jamii.

Kwa mfano, katika riwaya hii ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*, mwandishi anaelezea kuhusu mila na desturi zinazohusu tambiko la kuomba mvua. Katika tukio hilo tambiko linaenda sambamba na utoaji wa sadaka kwa Mungu mkuu kupitia kwa mahoka. Katika kutekeleza mila hii, kuku mweusi alichinjwa kama sadaka. Mathalani, katika dondoo hapo chini, mwandishi anaonesha jinsi maombi yanavyofanyika kwa kuzingatia mahusiano ya kidarajia kupitia mwana wa lihoka ambaye ndiye ameteuliwa kupeleka dua hiyo. Maombi hayo yanapofanyika, wanataja mahoka ambao ni wawakilishi wao wanaowapeleka dua zao kwa Mungu mkuu aliye chanzo kikuu cha Nguvu-uhai. Katika jamii za Kiafrika mahoka huheshimiwa na hutumiwa na binadamu katika kutatua changamoto. Mnenuka (2020) anaeleza kuwa mahoka (wahenga) huwa na dhima ya kuunganisha watu na Mungu ambaye yupo mbali na binadamu lakini yupo jirani na mahoka (wahenga). Katika kudhihirisha mahusiano hayo mwandishi anatumia kupitia dondoo lifuatalo hapa chini:

“Mahoka mlio wa Kyala, msisikitike.
Mkisikitika ninyi hata Kyala husikitika pia;
Ndipo hutushushia maradhi mengi.
Leo wote tumekusanyika mbele yenu,
Ili kutoa sadaka ya maombi.
Tunamuomba Mbelekayi, mwenzi wenu,
Ambaye tumemchagua leo awe mshenga wetu,
Apeleke sadaka yetu mbele ya Kyala,
ili atujalie mvua, atujalie tele ya chakula,
Atujalie na uzima, tuweze kunyosha shingo (kulala)
Daima na salama. Sote tu wanae” (uk.17).

Katika dondoo hiyo kukubaliwa kwa sala (dua) yao kunategemea mahusiano yaliyopo baina ya mahoka na Mungu aliye nguvu kuu. Mwandishi anaonesha namna sala na sadaka zinavyotolewa na kukubaliwa na Mungu kupitia kwa mahoka. Kwa hiyo, muunganiko huo wa kidarajia wa nguvu mbalimbali unadhihirisha kukubaliwa kwa maombi. Hali hiyo tunaiona katika dondoo lifuatalo mwandishi anaposema:

...Tulifungua banda na kuingia inavyompasa kuhani mchaji. Tulikwenda moja kwa moja mpaka pembe tukufu. Kwa uangalifu mkubwa baba aliinama na kuangalia kama zilikuwepo ishara kwamba Kyala na Mahoka wameipokea sadaka yetu. Punde si punde baba akaniambia, “mwanangu, tushukuru. Sadaka yetu imepokelewa.”...Siafu wamekuja kula makombo ya

mhanga waliyobakisha mahoka. Hata wachache wao wameshiba na kufia ndani ya nyama. Aidha, kuna alama za kitu kimepita juu ya unga na kubutua ile ncha ya unga ambayo jana ilichongoka sana. Hii pia ni ishara kwamba, mshenga wetu Mbelekayi amekuja na kuchota sehemu ya unga (uk.18).

Mwandishi anatumia mila na desturi katika kuonesha namna Nguvu-uhai inavyofanya kazi kidarajia kama inavyoonekana katika dondoo hapo juu. Pia, anaeleza ishara mbalimbali ambazo ni kiashiria cha kukubaliwa kwa maombi. Kwa mantiki hiyo, mahoka wanaotajwa katika dondoo hiyo wanaonekana ndio wenye wajibu wa kulinda na kutatua changamoto za watu. Ili wanajamii waendeleo kulindwa wanapaswa kuwaheshimu mahoka. Mahoka wanatumika kama kiunganishi kati ya Mungu na wanadamu. Mwandishi anapotaja mahoka katika Ontolojia ya Kiafrika anadhihirisha wazi jinsi wanavyoonekana kuwa karibu na Mungu na kutudhihirishia Nguvu-uhai yao. Mahoka wanatumika kama wawakilishi tu ambao wanaombwa ili wasaidie kupeleka dua kwa Kyala (Mungu). Pia, hata Mbelekayi anayetajwa katika nukuu hiyo ni mzee ambaye amechaguliwa kupeleka maombi kwa mahoka. Katika jamii za Kiafrika inaaminika kuwa wazee wenye umri mkubwa wana Nguvu-uhai kubwa kwa sababu wanaelekea kuwa wahenga (Wiredu, 1980). Kupitia mhusika Mbelekayi mwandishi anathibitisha anaposema: ‘Tazama, watu wako waomba mvua, wamenichinjia kuku. Kumbe mimi sina mamlaka ya kuwapa mvua, hivi tafadhali uwajalie mvua’ (uk. 19). Katika sentensi hizo maelezo yanayotolewa na mwandishi yanadhihirisha udarajia wa Nguvu-uhai unavyotenda kazi katika Ontolojia ya Kiafrika.

Halikadhalika, mila na desturi zimesawiriwa katika masuala ya misiba na taratibu za mazishi. Katika miktadha hii, inaaminika kuwa iwapo marehemu hajatendewa vizuri wakati wa mazishi anaweza kuwarudia ndugu zake na kuwadhuru. Hali hii inatokana na sababu kuwa Waafrika wanaamini kuwa mfu anabadilisha mazingira yake ya kijiografia tu, kwani huendelea kuwako katika ulimwengu mwingine. Kutokana na imani hii, Waafrika huzingatia mila na desturi fulani wakati wa shughuli zote za msiba ili kuendelea kuimarisha Nguvu-uhai. Mwandishi analithibitisha hili anaposema:

Kisha kuosha nilitwaa vipingili sita vya mtumbitumbi kadiri wanavyoamuru wahenga. Vipingili viwili nilimpachika marehemu kati ya kidole gumba na kidole cha shahada, na kumwambia babangu marehemu kwa machozi mengi,
 “Baba, kwa heri. Tangu leo umeacha mambo yote ya dunia.”
 Vipingili viwili nilimtia masikioni huku nasema,
 “Baba, kwa heri. Tangu leo hutasikia tena mambo ya duniani.”
 “Baba kwa heri. Tangu leo hutatembea tena duniani.”
 “Baba, tumekufunga mikono na miguu;
 Tumekuziba na masikio tupate kustarehe.
 Tutembe ulikotembea, tafadhali usitusumbue,
 Wala usikoroge usingizi wetu” (uk. 106-107).

Katika dondoo hii, Furata anatekeleza mila hii inayohusisha mambo yatakayotokea iwapo hawatatimiza mila na desturi za mazishi. Jambo hili la kuzingatia mila na desturi za mazishi linathibitishwa na Sanga (2020) anayeeleza kuwa kutowahifadhi na kuwahudumia marehemu ipasavyo kunaweza kuwaletea matatizo kadhaa katika jamii. Matatizo hayo ni pamoja na kutangatanga kwa mizimu ambayo huweza kuchukua na kuleta matatizo kwa ndugu zao. Ili kukwepa kadhaa hizo mila na desturi huzingatiwa. Kutokana na imani hii mahusiano ya waliokufa na walio hai huendelezwa kupitia mila na desturi zilizowekwa na miundo ya jamii. Mbiti (1969) anaeleza kuwa iwapo taratibu za mazishi hazikufuatwa kuna baadhi ya mizimu huweza kuwarudia na kuwadhuru wanadamu walio hai. Waafrika wanaamini kwamba watu waliokufa wanadumisha na kuendeleza

mahusiano yao na walio hai (Mbiti, 2000). Uhusiano huo ni wa ndani ni wa kiontolojia. Kwa Waafrika, kutomtendea vizuri aliyekufa kunaweza kuhatarisha maisha ya wanaobaki.

Maadili

Mbali na mila na desturi zinazosawiriwa na riwaya hii ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*, kadhalika kipengele cha maadili kinafungamanishwa na Nguvu-uhai. Katika jamii za Kiafrika suala la maadili linazingatiwa sana kwa sababu inaaminika kuwa huweza kuongeza au kupunguza Nguvu-uhai. Maadili hayo huhusu vipengele mbalimbali kama ukweli, usalama, upendo, haki, kuheshimu wengine na mali zao, kutunza makubaliano, kutimiza wajibu katika jamii na umoja.

Kwa Waafrika suala la maadili ni la kiontolojia, kwa minajili hiyo, mtu kwa tabia zake anaweza kusababisha furaha au huzuni kwa mwingine. Hivyo, inaaminika kwamba, kuwa na furaha au huzuni ni suala linalohusu kuimarika au kudhoofika kwa Nguvu-uhai. Chuachua (2016) anathibitisha suala hili anapoeleza kuwa kadri mtu anavyotenda mambo kinyume na maadili na itikeli, ndivyo anavyokuwa mbali na ukamilifu wake. Anaeleza kuwa thamani ya mtu huonekana kupitia matendo yake. Kwa hiyo, kiwango cha kuwa mtu, 'si mtu' huongezeka kulingana na kudhoofika kwa Nguvu-uhai. Chuachua anaeleza zaidi kuwa hali hiyo ni kinyume chake ikiwa mtu anatenda kulingana na matakwa ya kimaadili na kiitikeli. Kwa mfano, katika makala haya suala la maadili limesawiriwa kupitia mhusika Furata alipoambiwa na baba yake Keremkere atafute mchumba wa kuoja mwenye maadili. Mwandishi anasema:

“Furata mwanangu,
Wakati wako umewadia,
Tafuta moto.
“Nataka uoe binti ya watu,” aliongeza baba.
Msichana mwanana, mwanamwali mchaji.
Naam, bibi azizi.
Kigoli ajilondoshaye haramu.
Napenda nikufungie nikaha mwanangu wa pekee” (uk. 51).

Katika muktadha huu, Furata anaelekezwa mchumba apaswaye kumuoa, kuwa anapaswa kuoja mwanamke mwenye maadili. Maadili hayo ni pamoja na kumcha Mungu na kuheshimu wahenga. Suala la maadili linazingatiwa sana kutokana na mtazamo kwamba binadamu kama kiumbe hawezi kuishi peke yake, anajihusisha na viumbe wengine kwa sababu viumbe vyote vinahusiana. Kwa mantiki hiyo, iwapo atakosa maadili kwa kutokuishi kama jamii inavyotaka anaweza kuvuruga mahusiano hayo ambayo yanajumuisha walio hai na wafu. Kwa Waafrika, maadili yana mfungamo mkubwa sana na Mungu ambaye ndiye Nguvu-uhai kuu. Masolo (2011) anaeleza kwamba maadili hayawezi kutenganishwa na ontolojia pamoja na muunganiko wa viumbe unaofanywa na mwingiliano wa Nguvu-uhai. Thamani ya maisha inahusishwa na Mungu kama ndiye anayesababisha, kuyaimarisha na kuyalinda. Kwa viumbe wote, maisha ni Nguvu-uhai; kwa hiyo, kumtendea kinyume mwingine ni kuidhoofisha Nguvu-uhai yake.

Aidha, suala la maadili linaenda sambamba na umuhimu wa ubikira kwa mwanamke. Mwanamke aliyetunza bikira yake mpaka siku ya harusi huhesabiwa kuwa na maadili, bali asiyekuwa na bikira huhesabiwa kuwa muovu. Suala la bikira limeelezwa na mwandishi wakati familia ya akina Furata ilipotaka kujua iwapo msichana anayetaka kumuoa kama bado ni bikira. Mwandishi anathibitisha katika dondoo hapa chini kuwa:

Wazazi wangu hawakutaka niwalettee kahaba kuwa mkwe wao. Walipenda kigoli, bikira safi. Mwenye ujuzi wa kazi za nyumbani, bibi mwaminifu na wa kuweza kutegemewa. Hawakutaka nipose mzimu, bali bibi anayetambua daraja yake akastahi na utu wake. Naam, bibi azizi! (uk. 52).

Katika muktadha huu, bikira huchukuliwa kuwa moja ya amali ya msingi ya kimaadili katika jamii za Kiafrika. Katika jamii hii mwanamke asiye bikira ni aibu kwake na familia yake kwani huonekana kuwa hajaadilishwa. Mbiti (2000) anathibitisha suala hili kuwa mwanamke aliyetunza bikira yake mpaka wakati wa kuolewa huheshimiwa na kusifiwa kuwa na maadili mema. Kwa hiyo, mwanamke asiye bikira huwa ni aibu kwake na familia yake kwani huonekana kuwa hajaadilishwa. Mbiti anaeleza kuwa hapo zamani wanawake waliokutwa hawana bikira ndoa zao zilibatilishwa na wengine kuuwawa. Katika riwaya hii, ubikira ulikuwa unapimwa na kuthibitishwa kwa kupitia mila ambazo, zilimtaka binti kutimiza kaida fulani. Kama binti alibainika kuwa si bikira basi wazazi wake walipaswa kuomba radhi mapema kwa wazazi wa mwanaume. Mwandishi anaeleza:

“Dada wenye nyumba wataka uwathibitishie uzuri wa mwenendo wako. Wanadai kujua kama mwenendo wako ni adili, yaani, umeutunza vema ubikira wako mpaka hivi leo. Wapenda sasa uwape ishara wazi kuhusu neno hili. Basi unywe, hiki kilali.” ...Iwapo kweli siku zote umelinda ubikira wako hapo usione shaka kunywa hicho kilali. Hutadhurika kitu. Bali kama wewe si bikira, basi usithubutu kukinywa wala kukigusa tu... Bi Riha alikipokea kilali na kukinywa mara, hata baada ya dakika kumi zaidi, baada ya kumshika shika hapa na pale, bibi Parama alipaza kigelegele cha ushindi. “Tumepata bibi adili,” mwali bikira safi... “Mkwe wenu ni bikira safi.” (uk. 61-62).

Katika dondoo hiyo, pia kuna matumizi ya dawa anayonyweshwa Riha, kama sehemu ya kiapo ili aungame ukweli. Dawa hiyo inahusishwa na nguvu fulani kuwa iwapo hatasema kweli, dawa hiyo ina nguvu inayoweza kumdhuru. Mambo mawili muhimu katika dondoo hii ni haya, ubikira ni ishara ya maadili mema. Pamoja na kiapo cha kunywa kilali ni ishara ya kuwa mkweli ambapo ukweli wa ubikira huo umedhihirika kwa kutokudhurika. Pia, matumizi ya moshi mweusi yanayotajwa katika dondoo hiyo katika kupima ubikira, yanathibitisha wazi kuwa ndani ya huo moshi kuna nguvu. Kiontolojia, moshi umetumika kupima ukweli wa ubikira kwa sababu katika jamii za Kiafrika vitu vina nguvu inayoweza kuleta matokeo fulani. Namna masuala ya maadili yanavyoelezwa na mwandishi yanaonesha wazi kuwa suala la maadili lina mfungamano mkubwa na masuala ya kiontolojia katika mtagusano wa nguvu mbalimbali.

Jamii za Kiafrika huchukua hadhari kubwa katika sekta ya ndoa kuhusu maadili, kwamba ndoa, familia na unyumba ni vitu visivyochezewa. Hivi ni vitu vinavyothaminiwa katika jamii na ndio sababu inatakiwa kuchukua tahadhari kubwa. Kusudi la ndoa ni kuendeleza Nguvu-uhai kupitia uzazi wa watoto. Kwa hivyo, ili kujenga ukoo mzuri ni lazima kuzingatia masuala ya maadili. Ndoa ni daraja linalounganisha mnyororo wa Nguvu-uhai. Walio hai na wafu huunganishwa na kuwa pamoja. Kizazi kilichopita kinawakilishwa na wazazi; kilichopo kinawakilishwa na maisha ya mtu anayoishi na kijacho kinaletwa kupitia uzazi wa watoto. Kwa njia hii, ndio maana maadili huzingatwa.

Afya

Kuwa na afya njema ni ishara ya kuimarika kwa Nguvu-uhai. Kwa Waafrika, mwanajamii anapougua utulivu na amani ya familia hupungua. Familia huhoji chanzo cha ugonjwa ili kuweza kutafuta suluhu. Kwa hiyo, suala la afya ni la kiontolojia na huhusishwa na nguvu mbalimbali ambazo zinaweza kuimarisha ama kudhoofisha afya ya mtu. Watu hai, wafu, viumbe na vitu mbalimbali vina nafasi kubwa katika kushughulika na afya ya mtu. Kuthibitisha suala hilo katika riwaya ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*, mwandishi amesimulia kisa kuhusiana na afya. Kisa hicho kimesimuliwa kupitia tukio la kuzaliwa Furata, ambapo mama Wingi anamsimulia Furata mwenyewe. Mwandishi anasema:

“Kwa muda wa miezi tisa hali yangu ilikuwa njema sana. Nilinenepa wastani, nikanawiri vema. Titi zangu zikawa mororo zenye kung’aa. Jirani wote wakasema, baraka

imenikalia vyema” (uk. 3).

Kimsingi maelezo hayo yanaelezea kuhusu suala la kuwa na afya njema. Afya njema hiyo inahusishwa moja kwa moja na nguvu ambazo kupitia kwazo mtu huweza kubarikiwa. Mawazo ya Waafrika kuhusu afya na uhusiano wake kiontolojia yanaendelezwa na Mwandishi anaposema:

“Wiki moja mbele ya kujifungua vioja vilizidi. Kila siku paka walilia kama wanadamu karibu na nyumba nilimolala. Kila siku babako aliota ndoto: alizaliwa mwana ambaye aliwanga wachawi wengi waliokuja ili wamwue. Mchana uliotangulia siku ya kujifungua mwigo aliimba kwa muda mrefu, ishara kwamba atafika mgeni nyumbani petu. Jioni yake palionekana *ndupuka*, nyoka asiye na kichwa wala mkia. Mara nyoka huyo alipotoweka mizuka ya shangazi yako ilibashiri kwamba kutapita msiba mkubwa baada ya siku mbili. Mambo hayo yote yalitia hofu kubwa na bumbuzi mioyoni mwa kila mtu aliyeyaona au kusikia” (uk.3-4).

Dondoo hiyo inaonesha matukio mbalimbali yaliyochagizwa na afya ya mama Wingi katika hali ya ujauzito. Suala la ishara na matukio mbalimbali yanayojitokeza yanahusishwa na nguvu mbalimbali halisi na zisizo halisi. Magesa (1997) na Nkemnkia (1999) wanaeleza kuwa ili uzazi ufanikiwe ni lazima wazazi wawe na maadili. Matukio mbalimbali yanayojitokeza katika tukio la kuzaliwa Furata kama milio ya paka na vioja vingine vinawaaminisha wakunga kuwa kuna maadili yamevunjwa. Hii ndiyo sababu wanataka mjamzito aungame. Waafrika wanaamini kuwa katika hali ya ujauzito na wakati wa kujifungua kunapotokea changamoto yoyote, huwa kuna mahusiano ya kiontolojia ambayo yamevurugwa. Ili kurekebisha hali hiyo basi wahusika hulazimika kufuata taratibu fulani ili kurekebisha. Mbiti (1969) anaeleza kuwa kutokana na mimba kuwa na thamani kubwa katika jamii za Kiafrika mama mjamzito hupewa umuhimu na uangalizi mkubwa ili kumlinda kiumbe na mama kutokana na hatari inayoweza kujitokeza wakati wa kujifungua na baada. Mwandishi anaonesha fikra hizo anaposema:

Fauka ya hayo wakunga walinipa maswali mengi, wakanidai kabisa niungame mbele yao kuhusu mwenendo wangu wa siku za ujana. Nilinyweshwa dawa bila kiasi, ati za *mapinga* ili kunijalia uzazi mwema. Aghalabu nilikaidi kuzinywa nikiogopa zitamdhuru mwanangu.... Mateso yalizidi siku hadi siku, nami nikawa nazidi kuwaomba mahoka: enyi mahoka muutazame unyonge wangu, mkaangalie ninavyochekwa. Mlinden mtoto wangu (uk.4).

Waafrika wanaamini kuwa kila taabu na mateso yanasababishwa na nguvu nyingine kutoka nje. Kadhalika, taabu hiyo inaondolewa na nguvu nyingine yenye nguvu zaidi. Inaelezwa kuwa ikiwa mwenendo wa mtu ni mbaya huweza kuwajibishwa kwa kuwa suala la afya ni la kiontolojia. Tukio la kuzaliwa Furata linaonesha bayana fikra hizo kutokana na changamoto anayoipitia mjamzito wakati wa kujifungua. Hivi ndivyo afya inavyofungamanishwa na Nguvu-uhai. Maelezo ya mwandishi yanathibitisha kuwa kwa Waafrika suala la afya ni mtambuka linalosimamiwa na nguvu mbalimbali katika darajia za Nguvu-uhai.

Uzazi

Uzazi kwa Waafrika unachukukiliwa kama tunu inayompa mtu heshima. Waafrika kuzaa huwafanya wathaminiwe. Mtu asipozaa heshima yake hupungua na wanajamii huwakejeli wasiozaa. Mbiti (2000) na Sosoo (2020) wanaeleza kuwa thamani ya wanandoa katika jamii za Kiafrika hutokana na wanandoa hao kupata watoto na kinyume chake wanakuwa na thamani ndogo. Kuheshimiwa na kutambuliwa kama mtu hai kwa Waafrika ni kupata watoto. Katika kuonesha tunu hiyo mwandishi

katika riwaya hii anaeleza jinsi familia ya Keremkere ilivyokuwa inakejeliwa na wanajamii baada ya kuishi takribani miaka kumi na tisa pasipo kupata uzazi. Mwandishi anaeleza:

Kwa miaka yapata kumi na tisa nyumba yetu ilijaa huzuni na masikitiko. Baadhi ya watu walizoea kutukejeli, na wengine kutosikitikia kwa sababu hatukuwa na mtoto. Hata tulichoka kusikia maswali yaleyale ya daima: eti, bwana Keremkere, nani atarithi mali zako? nani atadumisha ukoowako? (uk.1).

Kauli inayotolewa na mwandishi katika nukuu hii inadhihirisha wazi namna Waafrika wanavyothamini uzazi. Kuzaa huufanya ukoo udumu (Bujo, 1999). Hii ina maana kwamba hata mzazi anapofariki iwapo amezaa, watoto aliowazaa huendeleza ukoo. Ukoo unajengwa kwa uzazi ambao ndio msingi wa kuendeleza Nguvu-uhai.

Pia, mwandishi anabainisha jinsi suala la uzazi linavyofungamana na masuala ya kiontolojia. Anadhihirisha suala hili kupitia kwa familia ya Keremkere walipokuwa wanausaka uzazi. Anaeleza kuwa suala la msako wa uzazi linahusisha mifumo ya kiontolojia ambapo nguvu mbalimbali zinahusishwa ili uzazi uweze kufanikiwa. Mwandishi anasema:

Aidha, tuliwaendea waganga wa kuteta, tukatolea sadaka nyingi kwa Mulungu na mahoka wake. Hata nilipoelekea kukata tamaa babako alinihimiza: tusikate tamaa. Tumlilie Mulungu, huenda atasikiliza kilio chetu. Na kweli. Kifuku cha ishirini tangu tuoane, kwa mara ya kwanza nilichukua mimba. Nasi tukafurahi sana... (uk. 1).

Katika dondoo hii, inaonesha wazi jinsi mahusiano ya Kinguvu-uhai yalivyofanikisha kupatikana kwa uzazi. Mulungu (Mungu) ambaye ndiyo nguvu kubwa kupitia kwa mahoka walifanikisha suala la uzazi na hatimaye kupata mtoto. Kutokana na hilo, ni dhahiri kuwa kwa Waafrika nguvu hizo zinafanya kazi. Mungu ambaye ndiye kiini cha nguvu nyingine anafanya kazi na kuvipatia viumbe nguvu hata kumwezesha binadamu kufanikisha mahitaji yake.

Aidha, kutokana na thamani ya uzazi katika kuendeleza Nguvu-uhai baada ya mimba kupatikana ili kukamilisha suala la uzazi kama tulivyokwisha kueleza hapo awali, mila na desturi mbalimbali huzingatiwa ili kuendelea kulinda uzazi usipatwe na vikwazo au uharibifu. Kwa mfano, mama mjamzito huzuiwa kutumia baadhi ya vyakula au kutofanya vitu fulani kwa kuhofia kuwa vinaweza kudhoofisha Nguvu-uhai yake na mtoto aliye tumboni.

Kwa Waafrika kuzaa watoto wengi ni jambo linalothaminiwa kwa sababu kadri mtu anavyozaa watoto wengi, wazazi wanapata ufahari. Uzazi wa watoto wengi ni nguvu-kazi inayoongeza uzalishaji na pia ulinzi kwa wazazi pindi watakapozeeka na wao watakapozaa wataoa na kupanua ukoo. Akifafanua kuhusu uzazi wa watoto wengi Faustine (2017) anashajiisha hoja hii anaposema Waafrika wanaamini kuwa kuzaa watoto wengi ni baraka. Mwandishi katika riwaya hii anadhihirisha ufahari huo anapoeleza, 'Maana, mzee Madakata alikuwa na wake watano na watoto ishirini. Miongoni mwao kumi walikwisha oa' (uk. 34). Kwa mantiki hiyo, Nguvu-uhai kupitia uzazi huendelezwa kupitia mwendelezo wa vizazi. Ili watoto wawe wengi ndio maana Waafrika hupendelea kuoia wake wengi, ijapokuwa jambo hili linapigwa vita na baadhi ya imani za kidinikama Ukristo. Watoto ndio wanadumisha ukoo. Mbiti (2000) anaeleza kuwa kadri mtu anavyozaa watoto wengi ndivyo na heshima yake inavyozidi kuwa kubwa kwa jamii.

Uzazi unapotokea unaleta furaha si kwa familia tu bali pia kwa jamii nzima kwa sababu ni baraka ambayo itadumisha ukoo. Ugumba huchukuliwa kuwa ni laana na mauaji ya ukoo. Mwandishi anasema:

Mara moja babangu Keremkere na mamangu Wingu walipiga mbiu ya mgambo kila upande ili ndugu waandae karamu kubwa dunia haijapata kuiona bado.

'Bi Riha ana mimba''ilinena taarifa,

mke mwema wa mwana pekee. Naye Furata,...
“Tunataka”, iliendelea taarifa,
“Kualika Masoka nzima ije Kisarawanda,
Watu wapate kujua kwamba Kisarawanda kuna jema.
Kina dada waseme: Heri yake bi Riha kwamba amezwa
Kisarawanda.
Nao walio tasa waeleke jiwe kwa shangwe’... (uk.
96).

Nukuu hii, inaonesha jinsi jamii inavyofurahia uzazi. Kwa minajili hiyo kuzaliwa mtoto ni suala ambalo si la kifamilia, wala ukoo pekee bali linahusu jamii nzima. Ndio maana watu wanalifurahia kwa kunywa pombe, kucheza ngoma na kuimba kwa shangwe kwa kumtakia mzazi heri na uzazi mwema. Faustine (2017) anahititisha hili kuwa suala la umuhimu wa kuwa na watoto kwa Waafrika hudhihirika pia katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile sherehe za tohara na harusi ambapo wanajamii huimba nyimbo za kumsifia mzazi wa mtoto anayehusika katika shughuli hiyo na kuwabeza wale wasio na uwezo wa kuzaa. Sentensi inayosema “Nao walio tasa waeleke jiwe kwa shangwe” inadhahirisha ubezaji huo kwa wasiozaa.

Hitimisho

Makala hii, imedhihirisha kuwa Nguvu-uhai inahusu mambo mbalimbali katika jamii za Kiafrika ikiwa ni pamoja na mila na desturi, maadili, afya na uzazi. Baadhi ya maudhui mbalimbali ya Kiafrika huelezwa kupitia vipengele hivyo kama vile heshima kwa wakubwa, malezi ya watoto, kuzingatia maadili, kuheshimu mila, na mahusiano. Makala hii imeweka wazi kuwa ili kuelewa Nguvu-uhai kwa Waafrika ni lazima uilewe ontolojia yao. Waafrika Nguvu-uhai huonekana zaidi kupitia matendo na uzoefu wa maisha ya kila siku namna watu wanavyoishi. Makala hii ni fupi haijaweza kugusia vipengele vyote vya Nguvu-uhai. Hivyo, ipo haja ya kuandika makala nyingine kwa kuchunguza jamii ambazo fasihi yao haijahifadhiwa katika maandishi ili kupanua mawanda yake.

Marejeleo

- Agada, A. (2020). *The African Vital Force Theory of Meaning in Life*. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1080/02580136.2020.1770416>. Ilisomwa tarehe 5 Februari 2021.
- Bujo, B. (1999). *African Theology in its Social Context*. Nairobi: Paulines Publications.
- Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi Katika Mukadamba wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Faustine, S. (2017). *Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Uhalisia wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya za Kiswahili*. Tasnifu ya uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Lavenda, R. H. na Schultz, E. A. (2010). *The Core Concept in Cultural Anthropology*. New York: McGraw- Hill Publishers.
- Madumulla, J. S. (1988). “Bw. Myombokere na Bi. Bugonoka” Katika *Kiswahili* 55/1&55/2: Dares Salaam: TUKI, kur 182-195.
- Magesa, L. (1997). *African Religion: The Moral Traditions of Abundant Life*. New York: Orbis Books Publishers.
- Masolo, D. (2011). *African Philosophy in Search of Identity*. Nairobi: East African Publishers Ltd.
- Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*. New York: Praeger Publishers.
- Mbiti, J. (2000). *Introduction to African Religion* (Second Edition). Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mihanjo, A. (2004). *Falsafa na Usanifu wa Hoja-Kutoka Wayunani Hadi Watanzania (Waafrika)* Morogoro: Salvatorium Institute of Philosophy and Theology.
- Mihanjo, A. (2007). *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa: Toka Uyunani Hadi Afrika*. Morogoro: Salvatorium Institute of Philosophy and Theology.

- Mnenuka, A. (2020). "Mizimu katika Ngano za Kiafrika: Uchambuzi wa Ngano Teule" katika *Mulika* na. 39, Hans, M.M. na Kadallah, R. T. (Wah) Dar es Salaam: TATAKI: 1-19.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasibi ya Kiswabili: Kozi za Fasibi Vyuoni na Vyno Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Nalwamba, K. na Buitendag, A. (2017). *Vital Force as a Triangulated Concept of Nature and s(S)Pirit*. Pretoria: University of Pretoria.
- Ngangah, I.G. (2019). Vital Force, Personhood, and Community in African Philosophy. An Ontological Study. Inapatikana katika <https://doi.org/10.24940/theijhss/2019/v7/i10/HS/HS1910-023>. Ilisomwa Tarehe 25 Januari 2021.
- Nkemnkia, N. M. (1999). *African Vitalogy: A step Forward in African Thinking*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Nkweru, F. V. (1967). *Mzishi wa Baba Ana Radbi*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.
- P Bitek, O. (1970) *African Religions in Western Scholarship*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Sanga, T. J. (2021). "Dhima ya Mbolezi za Sasa katika jamii ya Wakinga." Katika *Kioo cha Lugha* na. 18 Mchepange, S.O na Kidami, R.P. (Wah) Dar es Salaam: TATAKI: 208-228.
- Smith, E. W. (1961). *African Ideas of God*. London: Edinburgh House Press.
- Sosoo, F. K. (2020). "Ushujaa katika Motifu ya Safari ya Msako na Utamaduni na Falsafa ya Kiafrika." katika *Kioo cha Lugha* na. 18. Mchepange, S.O na Kidami, R.P. (Wah) Dar es Salaam: TATAKI: 152-171.
- Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.
- Tugendhat, E. (2016). *Traditional and Analytical Philosophy*. Cambridge: University Printing House.
- Tylor, E.B. (2010). *Primitive Culture*. New York: Cambridge University Press.

